JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA

MKAKATI WA UTEKELEZAJI WA SERA YA MAENDELEO YA JASIRIAMALI NDOGO NA ZA KATI YA MWAKA 2003 (TOLEO LA MWAKA 2025) KWA KIPINDI CHA 2025/26 – 2034/35

2025

MKAKATI WA UTEKELEZAJI WA SERA YA MAENDELEO YA JASIRIAMALI NDOGO NA ZA KATI YA MWAKA 2003 (TOLEO LA MWAKA 2025) KWA KIPINDI CHA 2025/26 – 2034/35

YALIYOMO

YALIYOMO ..... ii-iii
VIFUPISHO ..... iv-v
UFAFANUZI WA MANENO vi
SURA YA KWANZA 1
1. UTANGULIZI 1
1.1. Usuli 1
1.2. Utekelezaji wa Vipaumbele vya Kimkakati 1
1.3. Majukumu na Wajibu wa Wadau 2
1.4. Matokeo Yanayotarajiwa 2
1.5. Hitimisho 2
SURA YA PILI 3
2. UCHAMBUZI WA HALI ILIVYO NA UMUHIMU WA SERA 3
2.1. Uchambuzi wa Hali ilivyo 3
2.1.1. Mfumo wa Kisheria 3
2.1.2. Miundombinu Wezeshi 4
2.1.3. Huduma za Uendelezaji Jasiriamali 4
2.1.4. Teknolojia na Ubunifu 5
2.1.5. Upatikanaji wa Masoko 5
2.1.6. Huduma za Kifedha katika Biashara 6
2.1.7. Uanzishaji na Uendelezaji wa Viwanda Vijijini 7
2.1.8. Uendelezaji Jasiriamali 8
2.1.9. Masuala Mtambuka 9
2.2. Umuhimu wa kufanya marekebisho 12
SURA YA TATU 13
3. DIRA, DHAMIRA NA MALENGO 13
3.1. Dira na Dhamira 13
3.1.1. Dira 13
3.1.2. Dhamira 13
3.2. Malengo ya Sera 13
3.2.1. Lengo Kuu 13
3.2.2. Malengo Mahususi 13
SURA YA NNE 14
4. MALENGO, MIKAKATI NA SHABAHA 14
4.1. Miundombinu Wezeshi 14
4.2. Uendelezaji Jasiriamali 14
4.3. Teknolojia na Ubunifu 15
4.4. Upatikanaji wa Huduma za Kifedha 16
4.5. Upatikanaji wa Masoko 16
4.6. Masuala Mtambuka 17
SURA YA TANO 18
5. MPANGO WA UTEKELEZAJI 18
5.1. Utangulizi 18
5.2. Rasilimali Fedha 18
5.3. Muda wa Utekelezaji 18
SURA YA SITA 26
6. MFUMO WA KITAASISI, UFUATILIAJI NA TATHMINI 26
6.1. Mfumo wa Kitaasisi 26
6.2. Majukumu ya Wadau katika Utekelezaji wa Sera 26
SURA YA SABA 28
7.1. Utangulizi 28
7.2. Lengo kuu 28
7.3. Walengwa 28
7.4. Mipango ya Ufuatiliaji, Mapitio na Tathmini 28
7.4.1. Mpango wa Ufuatiliaji 28
7.4.2. Mpango wa Mapitio 29
7.4.2.1. Mpango wa Mapitio ya Viashiria vya Muda Mfupi 29
7.4.3. Mpango wa Tathmini 29
7.4.4. Mpango wa utoaji taarifa 33
7.4.4.1. Mpango wa utoaji taarifa ndani ya Wizara 33
7.4.4.2. Mpango wa utoaji taarifa nje ya Wizara 33
7.5. Ukusanyaji na Uchambuzi wa Data 33
7.6. Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini 33
7.6.1. Aina za taarifa za ufuatiliaji na tathmini 33
7.6.2. Ratiba ya utoaji taarifa 34
7.6.3. Mfumo wa utoaji taarifa 34
7.6.4. Mfumo wa kutoa mrejesho 34
7.7. Matumizi ya Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini 34
7.8. Mpango wa Utekelezaji 35
7.9. Hitimisho 35

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 1: Bangokitita la Mpango wa Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jasiriamali Ndogo na za Kati ya Mwaka 2003 (Toleo la mwaka 2025) 19
Jedwali Na 2: Viashiria vya Ufuatiliaji na Tathmini 30

VIFUPISHO

AfCFTA	Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika
AGCOT	Ushoroba wa Ukuzaji Kilimo Tanzania
ASDP	Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo
AZAKI	Asasi za Kiraia
AZISE	Asasi Zisizo za Serikali
BDS	Huduma za Maendeleo ya Biashara
BEST	Programu ya Uimarishaji wa Mazingira ya Biashara Tanzania
BOT	Bank Kuu ya Tanzania
BRELA	Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni
COSTECH	Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia
CAMARTEC	Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini
DITF	Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam
EAC	Jumuiya ya Afrika Mashariki
LGAs	Mamlaka za Serikali za Mitaa
MDAs	Wizara, Idara na Wakala za Serikali
MIVARF	Miundombinu ya Masoko; Uongezaji Thamani wa Mazao na Uboreshaji wa Huduma za Kifedha Vijijini
MKUMBI	Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara
MOF	Wizara ya Fedha
MOH	Wizara ya Afya
MOICT	Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari
MOT	Wizara ya Uchukuzi
MUVI	Muunganisho Ujasiriamali Vijijini
NCDs	Magonjwa Yasiyoambukizwa
NEEC	Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi
NFIs	Taasisi zisizo za Kifedha
NGDS	Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Jinsia
OMR	Ofisi ya Makamu wa Rais
OWM KAM	Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira na Mahusiano
POPI	Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji
REA	Wakala wa Nishati Vijijini
RUWASA	Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini
SACCOS	Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo
SADC	Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika
SIDO	Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo
TACAIDS	Tume ya UKIMWI Tanzania
TAMISEMI	Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
TANTRADE	Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania
TARURA	Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini
TCRA	Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania
TEHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
TEMDO	Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania
TIRDO	Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania
TPSF	Shirikisho la Sekta Binafsi Tanzania
VVU/UKIMWI	Virusi vya Upungufu wa Kinga Mwili/Upungufu wa Kinga Mwilini
MOW	Wizara ya Ujenzi
WVB	Wizara ya Viwanda na Biashara

UFAFANUZI WA MANENO

<table>
<tr><td>Mjasiriamali</td><td>Mtu mwenye hamasa na uwezo wa kuanzisha, kusimamia, na kufanikisha biashara huku akikabiliana na vihatarishi vinavyohusiana na biashara hiyo.</td></tr>
<tr><td>Ujasiriamali</td><td>Uwezo na utayari wa kuanzisha, kupanga, na kuendesha biashara pamoja na kukabiliana na changamoto zake zote kwa lengo la kupata faida.</td></tr>
<tr><td>Jasiriamali</td><td>Shughuli ya kiuchumi inayozalisha bidhaa au huduma kwa lengo la kupata faida.</td></tr>
<tr><td>Ukuaji wa Biashara</td><td>Mabadiliko chanya katika ukubwa wa biashara kwa kuzingatia mauzo, faida, mali, uzalishaji na soko.</td></tr>
<tr><td>Uendelezaji Jasiriamali</td><td>Mchakato wa kuanzisha na kuboresha thamani ya biashara, taswira na kukuza mtaji.</td></tr>
<tr><td>Sekta isiyo rasmi</td><td>Shughuli au rasilimali inayomilikiwa bila kuwa na usajili maalumu kisheria, bila kuwa na leseni ya uendeshaji iliyosajiliwa na mamlaka za Serikali za mitaa au wizara za kisekta.</td></tr>
<tr><td>Huduma za Uendelezaji Jasiriamali</td><td>Huduma zisizo za kifedha zinazotolewa kwa wajasiriamali ili kuboresha uendeshaji na tija katika biashara.</td></tr>
<tr><td>Jasiriamali Ndogo Sana, Ndogo na za Kati</td><td>Shughuli halali za kiuchumi zisizo za kilimo (yaani uzalishaji viwandani, uchimbaji madini, biashara na huduma) ambazo zimeainishwa kama ifuatavyo:
<table>
<tr><th>Daraja</th><th>Sekta</th><th>Idadi ya Wafanyakazi</th><th>Mtaji kwa Shilingi</th></tr>
<tr><td rowspan="3">Jasiriamali ndogo sana</td><td>Biashara</td><td>< 5</td><td>< 50 million</td></tr>
<tr><td>Huduma</td><td>< 5</td><td>< 50 million</td></tr>
<tr><td>Uzalishaji viwandani</td><td>< 20</td><td>< 100 million</td></tr>
<tr><td rowspan="3">Jasiriamali ndogo</td><td>Biashara</td><td>5 – 50</td><td>milioni 50 - bilioni 1</td></tr>
<tr><td>Huduma</td><td>5 – 50</td><td>milioni 50 - bilioni 1</td></tr>
<tr><td>Uzalishaji viwandani</td><td>20 - 100</td><td>100 milioni - 2 billion</td></tr>
<tr><td rowspan="3">Jasiriamali za kati</td><td>Biashara</td><td>>50-100</td><td>> bilioni 1 - bilioni 5</td></tr>
<tr><td>Huduma</td><td>>50-100</td><td>> bilioni 1 - bilioni 5</td></tr>
<tr><td>Uzalishaji viwandani</td><td>>100-300</td><td>> bilioni 2 - bilioni 10</td></tr>
<tr><td rowspan="3">Jasiriamali kubwa</td><td>Biashara</td><td>> 100</td><td>> bilioni 5</td></tr>
<tr><td>Huduma</td><td>> 100</td><td>> bilioni 5</td></tr>
<tr><td>Uzalishaji viwandani</td><td>> 300</td><td>> bilioni 10</td></tr>
</table></td></tr>
</table>

Tanbihi:
Neno *'Jasiriamali Ndogo'* linajumuisha pia jasiriamali ndogo sana.
Neno *'Mtaji'* unajumuisha fedha taslimu, bidhaa ghafi, bidhaa zilizozalishwa na ama miundombinu ya uzalishaji.

SURA YA KWANZA

1. UTANGULIZI

1.1. Usuli

Tanzania ina zaidi ya jasiriamali milioni 6 zenye kuajiri takriban watu milioni 11. Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine, imekuwa ikitekeleza Sera ya Maendeleo ya Jasiriamali Ndogo na za Kati ya mwaka 2003 kwa lengo la kuimarisha utendaji na ushindani wa kibiashara wa jasiriamali zilizopo na kuwezesha uanzishaji wa jasiriamali mpya. Utekelezaji wa sera hii umechochea kuibuka kwa idadi kubwa ya wajasiriamali wanaoshiriki katika shughuli za kibiashara, jambo ambalo limekuwa na mchango chanya katika jitihada zilizowezesha kufikiwa kwa malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025.

Kuongezeka kwa biashara changa na kukua kwa tasnia ya ubunifu; kuongezeka kwa matumizi ya TEHAMA katika shughuli za ujasiriamali; na mabadiliko katika viashiria vya uchumi jumla vilivyoleta haja ya kupanga upya madaraja ya jasiriamali vilileta changamoto katika utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jasiriamali Ndogo na za Kati ya mwaka 2003 na hivyo kuhitaji mapitio ya Sera. Ili kukabiliana na changamoto hizo, Serikali iliamua kupitia upya Sera ya Maendeleo ya Jasiriamali Ndogo na za Kati ya mwaka 2003 na kupata toleo la mwaka 2025. Utekelezaji wa maudhui ya toleo jipya la Sera utaimarisha na kuwezesha jasiriamali ndogo na za kati na kuzifanya kuwa endelevu na hivyo kuzifanya zitoe mchango mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi.

Utekelezaji madhubuti wa Sera ya Maendeleo ya Jasiriamali Ndogo na za Kati ya mwaka 2003 (Toleo la mwaka 2025) ulihitaji mkakati wa utekelezaji ambao unabainisha mikakati ya utekelezaji wa malengo ya sera; wadau watakaohusika; na rasilimali zinazohitajika katika utekelezaji.

Mkakati huu utatekelezwa kwa kipindi cha miaka 10 kuanzia mwaka 2025 hadi mwaka 2035. Utekelezaji umejikita katika malengo sita (6) ya kisera. Katika Mkakati huu wa Utekelezaji wa Sera, kila eneo lina mikakati na shabaha zitakazofikiwa baada ya utekelezaji.

1.2. Utekelezaji wa Vipaumbele vya Kimkakati

Maeneo ya kipaumbele yaliyoainishwa katika utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jasiriamali Ndogo na za Kati ya mwaka 2003 (Toleo la mwaka 2025) ni pamoja na uendelezaji wa miundombinu wezeshi; uendelezaji jasiriamali; teknolojia na ubunifu; upatikanaji wa huduma za kifedha; upatikanaji wa masoko; na ujumuishaji wa masuala mtambuka (mazingira, jinsia na vijana, watu wenye ulemavu, VVU/UKIMWI, utawala bora na magonjwa yasiyoambukizwa) katika shughuli za uendelezaji jasiriamali. Maeneo haya ya kipaumbele yanatarajiwa kuchochea ukuaji wa shughuli za ujasiriamali na kuongeza mchango wake katika maendeleo ya uchumi.

1.3. Majukumu na Wajibu wa Wadau

Utekelezaji wa sera hii unahitaji ushirikiano wa wadau mbalimbali katika ngazi za kitaifa, kikanda, na kimataifa. Watekelezaji wakuu wa Sera hii ni wizara yenye dhamana ya uendelezaji wa jasiriamali; wizara za kisekta; idara na wakala wa serikali; sekretarieti za mikoa; na mamlaka za serikali za mitaa. Wadau wengine ni washirika wa maendeleo; taasisi za elimu na utafiti; sekta binafsi; asasi zisizo za serikali; asasi za kiraia; vyombo vya habari; na jamii kwa ujumla. Wadau hawa watakuwa na majukumu na wajibu muhimu katika utekelezaji wa Sera hii kupitia utafiti; utetezi; uhamasishaji; ufuatiliaji; utafutaji wa rasilimali; na kujenga uwezo wa wajasiriamali.

1.4. Matokeo Yanayotarajiwa

Utekelezaji wa sera iliyopitiwa utawezesha upatikanaji wa miundombinu wezeshi kwa ajili ya shughuli za ujasiriamali ambazo zitasaidia kuongezeka kwa bidhaa na huduma. Aidha, utaimarisha mfumo wa usafirishaji wa bidhaa kwa kuunganisha wajasiriamali katika ngazi za kitaifa, kikanda na kimataifa na hivyo kuongeza wigo wa masoko ya bidhaa na huduma. Vilevile, utekelezaji wa Sera utawezesha upatikanaji na utumiaji wa huduma za kifedha na zisizo za kifedha zitakazowezesha wajasiriamali kuongezeka na kukuza biashara zao. Pia, utekelezaji wa Sera utaongeza matumizi ya teknolojia itakayowezesha kukuza ubunifu katika uzalishaji na hivyo kuongeza ubora na uanuwai wa bidhaa na huduma.

1.5. Hitimisho

Mkakati huu unaweka msingi utakaowezesha utekelezaji wa Sera kufanyika kwa ufanisi ili kukidhi matarajio ya wadau. Hivyo, kupitia utekelezaji wa mkakati huu taifa litashuhudia ukuaji madhubuti wa shughuli za ujasiriamali ambazo zitachochea uzalishaji wa ajira, kuongezeka kwa kipato na kupunguza umasikini.

SURA YA PILI

2. UCHAMBUZI WA HALI ILIVYO NA UMUHIMU WA SERA

2.1. Uchambuzi wa Hali ilivyo

Sera ya Maendeleo ya Jasiriamali Ndogo na za Kati ya mwaka 2003 ilijikita katika maeneo makuu saba ambayo ni Mfumo wa Kisheria, Miundombinu Wezeshi, Huduma za Maendeleo ya Biashara (zikiwamo maendeleo ya ujasiriamali, mafunzo ya biashara, upatikanaji wa taarifa, teknolojia na masoko), Upatikanaji wa Huduma za Fedha, Mfumo wa Kitaasisi wa Maendeleo ya Jasiriamali Ndogo na Kati, Uanzishwaji na Uendelezaji wa Viwanda Vijijini na Masuala Mtambuka (yakiwamo masuala ya mazingira, jinsia, makundi maalumu, VVU/UKIMWI na magonjwa yasiyoambukizwa). Ufuatao ni uchambuzi wa kina unaobainisha utekelezaji, mafanikio na changamoto zilizopo katika kila eneo.

2.1.1. Mfumo wa Kisheria

Mfumo wa kisheria unalenga kuweka mazingira yanayofaa kwa uendeshaji wa shughuli za kibiashara. Katika jitihada za kuboresha mazingira ya biashara, Serikali ilianzisha Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI) ambao ulichangia sana kuboresha hali ya biashara nchini Tanzania. MKUMBI umewezesha kuondolewa na kupunguzwa kwa ada na tozo mbalimbali. Mathalani, kati ya mwaka 2017/18 na 2022/23, Serikali ilifanya marekebisho ya kuondoa na kupunguza jumla ya ada 374 katika mamlaka mbalimbali za udhibiti. Jitihada nyingine zilizofanyika ni pamoja na kuanzishwa kwa Mfumo wa Usajili wa Biashara Mtandaoni unaosimamiwa na BRELA; uunganishaji wa usajili wa biashara na Kanzidata ya Kitambulisho cha Taifa; na marekebisho ya sheria za kodi kupitia Sheria ya Fedha ya 2017/2018/2019.

Vilevile, ili kutoa fursa ya ushiriki jumuishi wa jasiriamali ndogo na za kati katika minyororo ya thamani ya kiuchumi katika sekta mbalimbali, Serikali ilitunga Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 10 ya mwaka 2023 ambayo inailazimu Serikali kutenga asilimia 30 ya zabuni zake za ununuzi kwa ajili ya wajasiriamali wadogo na wa kati. Serikali pia imetunga Sheria ya Usuluhishi ya mwaka 2020, ambayo imeweka mfumo wa kisheria wa kutatua migogoro ya kibiashara ya wajasiriamali kwa usawa.

Licha ya mafanikio yaliyotajwa hapo juu, mfumo wa kisheria uliopo bado haujawawezesha kikamilifu wafanyabiashara wadogo na wa kati kuanzisha na kuendesha biashara zao kwa ufanisi. Hii ni kutokana na kuwapo kwa gharama kubwa za uendeshaji ambazo zinakwamisha ukuaji wa biashara changa na kupunguza kasi ya urasimishaji wake.

2.1.2. Miundombinu Wezeshi

Katika muktadha wa Sera hii, miundombinu wezeshi inahusisha maeneo ya biashara na majengo yanayowezesha wafanyabiasha wadogo na wa kati kufanya shughuli zao. Serikali imechukua hatua kadhaa zikiwamo kutenga na kuendeleza ardhi kwa ajili ya shughuli za wafanyabiashara wadogo na wa kati katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; kujenga na kuendeleza majengo ya viwanda 547 yenye huduma za umeme, mifumo ya maji taka, barabara na miundombinu ya mawasiliano kupitia Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO); na kujenga majengo 367 ya biashara kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo na wa kati. Vilevile, Serikali imeimarisha miundombinu wezeshi kwa kuboresha barabara za vijijini na mijini, reli, usafiri wa anga, mawasiliano, umeme, maji na huduma nyingine muhimu. Hatua hizo zimewawezesha wafanyabiashara wadogo na wa kati kuongeza tija na ushindani.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, bado kuna changamoto zinazowakabili wajasiriamali wadogo na wa kati ukiwamo upungufu wa majengo ya viwanda na vyumba na vifaa vya baridi vya kuhifadhia bidhaa; upungufu wa miundombinu wezeshi (usafirishaji, usambazaji na mifumo ya kupakia na kupakua mizigo, maghala, reli, bandari, viwanja vya ndege na TEHAMA) inayounganisha maeneo ya vijijini na mijini.

Changamoto hizo zinasababishwa na upatikanaji wa huduma usio wa uhakika (mifumo ya maji safi na maji taka, nishati, gesi); na gharama kubwa za kutumia miundombinu wezeshi kwa wafanyabishara wadogo na wa kati. Matokeo ya changamoto hizo ni pamoja na kuongezeka kwa migogoro kati ya wafanyabishara wadogo na wa kati na mamlaka za mipango miji; kuongezeka kwa shughuli za wafanyabiashara wadogo na wa kati katika maeneo yasiyo rasmi; na mwitikio mdogo wa wajasiriamali kuanzisha biashara rasmi.

2.1.3. Huduma za Uendelezaji Jasiriamali

Huduma za uendelezaji jasiriamali zililenga kuwawezesha wajasiriamali wadogo na wa kati kupata ujuzi muhimu wa uendeshaji na usimamizi wa biashara. Sekta za umma na binafsi, pamoja na washirika wa maendeleo, walitekeleza programu muhimu za watoa huduma za maendeleo ya biashara katika maeneo mbalimbali, wakitoa maarifa na ujuzi muhimu kwa wajasiriamali. Moja ya mafanikio yaliyofikiwa ni kujumuisha mafunzo ya ujasiriamali katika taasisi zote za elimu ya juu na vyuo vya kati, hivyo kuongeza ari ya ujasiriamali miongoni mwa vijana. Mwaka 2013, Serikali ilizindua Mwongozo wa Taifa wa Mafunzo ya Ujasiriamali ili kuimarisha uratibu wa mafunzo ya ujasiriamali katika shule za msingi na sekondari.

Vilevile, Serikali ilianzisha vituo 24 vya uwezeshaji wananchi kiuchumi ambavyo viliratibu programu za mafunzo kwa wajasiriamali 16,119. Aidha, kupitia vituo hivyo, jumla ya biashara 16,489 zilirasimishwa, ambapo asilimia 57 ya biashara hizo zilikuwa zikimilikiwa na wanawake. Taasisi za umma, sekta binafsi na washirika wa maendeleo, hususan Shirikisho la Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), wamekuwa wakihamasisha shughuli za ujasiriamali kupitia mipango inayolenga kukuza ushindani. Kadhalika, TPSF imeanzisha mfumo wa kielekroniki wa kuratibu masuala ya ujasiriamali ili kuongeza ubunifu kwa wajasiriamali waliopo na wapya.

Vilevile, kupitia Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo wajasiriamali wamekuwa wakipatiwa mafunzo mbalimbali ya usimamizi na uendeshaji wa biashara. Katika kipindi cha miaka 10 kuanzia 2013/2014 hadi 2022/2023, jumla ya wajasiriamali 173,839 walipatiwa mafunzo hayo.

Licha ya jitihada hizo, wajasiriamali wadogo na wa kati nchini Tanzania wanakabiliwa na changamoto kadhaa zinazoathiri upatikanaji na utumiaji huduma za uendelezaji jasiriamali. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na uelewa mdogo kuhusu upatikanaji wa huduma hizo; wajasiriamali kutothamini umuhimu wa huduma za uendelezaji jasiriamali; kukosekana kwa huduma mahususi za kisekta; mifumo ya uratibu wa utoaji wa huduma za uendelezaji jasiriamali isiyo toshelevu; baadhi ya huduma kujikita mijini na kutowafikia wajasariamali wa vijijini; na kutokuwiana kati ya huduma zinazatolewa na mahitaji halisi.

2.1.4. Teknolojia na Ubunifu

Teknolojia na ubunifu ni muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi na kuwezesha ushindani kibiashara. Vilevile, huhusisha kubuni na kutumia teknolojia mpya au zilizoboreshwa ili kutatua matatizo, kuongeza ufanisi, na kuongeza thamani ya bidhaa na huduma. Serikali imekuwa mstari wa mbele katika kuwezesha upatikanaji na kuhimiza matumizi ya teknolojia; kukuza ushirikiano kati ya taasisi za utafiti na shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati; na kuanzisha mifumo ya kuboresha mtandao kati ya wajasirialiamali na watoa huduma za teknolojia.

Kutokana na jitihada hizo, mafaniko mbalimbali yamejitokeza ambapo wajasiriamali 7,651 walipewa mafunzo ya matumizi ya teknolojia 608 zilizobuniwa na SIDO. Aidha, taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (TEMDO) na Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC) zilibuni na kusambaza teknolojia 12 kwa wajasiriamali. Vilevile, programu 12 za viatamizi kwa wabunifu zilianzishwa kusaidia wajasiriamali wabunifu kuendeleza teknolojia zao ili ziweze kutumika katika kibiashara.

Licha ya mafanikio yaliyofikiwa, bado kuna kiwango kidogo cha matumizi ya teknolojia katika shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati. Hii inasababishwa na uhaba wa teknolojia na kiwango kidogo cha uelewa wa wajasiriamali kuhusu masuala ya haki miliki bunifu na matumizi ya teknolojia; uhaba wa tafiti; gharama kubwa za kupata teknolojia; na kukosekana kwa muunganiko baina ya watafiti na watumiaji wa teknolojia.

2.1.5. Upatikanaji wa Masoko

Serikali imeanzisha mikakati mbalimbali ili kuboresha upatikanaji wa masoko kwa huduma na bidhaa za wajasiriamali wadogo na wa kati, ikitambua umuhimu wake katika kupanua wigo wa wateja, kuongeza mapato, na fursa za ukuaji wa biashara. Miongoni mwa jitihada zilizofanyika ni kuandaa maonesho ya biashara na ziara za kibiashara ili kuwezesha wajasiriamali kuyafikia masoko ya ndani na ya kimataifa.

Jitihada hizo ziliwahamasisha wajasiriamali kushiriki kwa wingi katika maonesho mbalimbali. Mathalani, kupitia Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF) yanayoandaliwa na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) yamekuwa yakiwashirikisha wajasiriamali zaidi ya 500 kila mwaka.

Aidha, kupitia maonesho ya kitaifa yanayoratibiwa na SIDO zaidi ya wajasiriamali 1,320 wamekuwa wakishiriki kila mwaka. Aidha, kupitia maonesho ya SIDO kuanzia mwaka 2015 hadi 2025, wajasirimali walioshiriki katika maonesho hayo walifanikiwa kupata mauzo yenye thamani ya Tsh. 1,224,981,950 ikiwa ni pamoja na kuagizwa kuleta bidhaa zenye thamani ya Tsh. 1,754,890,900. Vilevile, kupitia maonesho ya JUA KALI yanayoandaliwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), jumla ya wajasiriamali 4,030 walishiriki maonesho hayo kuanzia mwaka 2004 hadi 2024 na kufanikiwa kupata mauzo yenye thamani ya Tsh. 12,123,000,000.

Katika jitihada za kuongeza thamani na bei ya mazao ya kilimo, Serikali ilitunga Sheria ya Stakabadhi za Ghala ya mwaka 2005 ili kuwezesha wafanyabiashara kutumia mfumo wa stakabadhi za ghala na kuwezesha uuzaji endelevu na wa haki kwa bidhaa zilizohifadhiwa kwenye maghala. Mfumo huu uliwanufaisha sana wajasiriamali wanaojihusisha na shughuli za kilimo na kuongeza thamani. Mathalani, mazao ya kilimo yaliyouzwa kupitia mfumo huu katika kipindi cha miaka 3 kuanzia 2021 hadi 2023 yaliongezeka thamani kwa zaidi ya asilimia 300 ikilinganishwa na mazao hayo yalipouzwa nje ya mfumo huo. Aidha, Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 10 ya mwaka 2023 inatoa upendeleo kwa wafanyabiashara wa ndani, ikiwamo wajasiriamali wadogo na wa kati, katika upatikanaji wa zabuni za Serikali. Sheria hii inalenga kuimarisha usimamizi wa ununuzi wa umma na kuhamasisha ushiriki wa wafanyabiashara wa ndani katika miradi ya Serikali.

Licha ya jitihada hizo, kiasi cha bidhaa za wajasiriamali zinazouzwa katika masoko ya ndani na ya kimataifa bado kipo chini. Hii inasababishwa na kukosekana kwa muunganiko madhubuti kati ya wajasiriamali wadogo na wa kati na makampuni makubwa kama wateja wa bidhaa zao; ujuzi mdogo wa masoko kwa wajasiriamali; na ubora mdogo wa bidhaa zinazozalishwa.

2.1.6. Huduma za Kifedha katika Biashara

Serikali imeweka mazingira bora ya kisera ambayo yanahamasisha ukuaji na uanzishwaji wa taasisi mbalimbali za kifedha zinazohudumia biashara zikiwamo jasiriamali ndogo na za kati. Hivi sasa, kuna zaidi ya taasisi ndogo za fedha 2,200 zinazotoa huduma kwa wakopaji wadogo, wengi wao wakiwa wajasiriamali wadogo na wa kati. Aidha, idadi ya asasi zisizo za serikali na kampuni ndogo zinazotoa huduma ya fedha zimeongezeka kutoka 9 mwaka 2002 hadi zaidi ya 292 mwaka 2016.

Vilevile, Serikali, kwa kushirikiana na wadau wengine imeanzisha mifuko 72 ya uwezeshaji wananchi ambapo kati ya hiyo 62 inasimamiwa na serikali na 10 inasimamiwa na sekta binafsi.

Baadhi ya mifuko hiyo ni Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Programu ya Uzalishaji Ajira; Mfuko wa SELF Microfinance; Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na Wanawake; Mfuko wa Uwezeshaji wa Mwananchi; Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali Wananchi na Mfuko wa Amana wa Rais.

Kupitia mifuko hiyo, katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2024, jumla ya Shilingi bilioni 743.7 zilikopeshwa kwa wajasiriamali 6,064,957 wakiwamo wanawake 3,288,186 na wanaume 2,776,771. Aidha, Serikali imeendelea kupunguza viwango vya riba kwa mikopo ya mifuko ya uwezeshaji ili kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa wananchi wengi zaidi. Kwa mfano, kiwango cha riba cha Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kimepungua kutoka asilimia 10 mwaka 2022 hadi kufikia asilimia 5 mwaka 2023/24. Vilevile, kiasi cha shilingi bilioni 430.5 kilitolewa kwa wanufaika 932,442 kupitia mifuko inayotoa mikopo ya moja kwa moja na dhamana. Vilevile, kiasi cha shilingi bilioni 313.2 kilitengwa kwa ajili ya wanufaika 5,132,515 kupitia mifuko inayotoa ruzuku.

Hali kadhalika, Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) vimechangia sana kufadhili wanachama wao, hasa wale wa biashara ndogo na changa. Idadi ya SACCOS zilizosajiliwa ilifikia 937 hadi mwaka 2024 hali inayoashiria kuboreshwa kwa mazingira ya kisera. Taasisi zisizo za kifedha (NFIs), ikiwemo waendeshaji wa mitandao ya simu (MNOs), zimekuwa na umuhimu mkubwa kwa wajasiriamali wadogo na wa kati, hususan katika kurahisisha miamala ya fedha.

Licha ya mafanikio hayo, bado kuna uhaba wa mitaji kwa wajasiriamali wadogo na wa kati kutokana na sababu mbalimbali. Sababu hizo ni pamoja na mikopo kuwa na riba kubwa; wajasiriamali kukosa dhamana rasmi; upungufu wa uanuwai wa huduma za mikopo zinazofaa kwa wajasiriamali wadogo na wa kati; na ukosefu wa ujuzi wa kutafuta mitaji na kusimamia mikopo.

2.1.7. Uanzishaji na Uendelezaji wa Viwanda Vijijini

Uanzishaji na uendelezaji wa viwanda vijijini unajumuisha shughuli za kiuchumi zinazofanyika vijijini ambazo hutofautiana kwa ukubwa kuanzia ngazi ya kaya hadi viwanda vidogo. Baadhi ya shughuli hizo ni usindikaji wa mazao ya kilimo, viwanda vidogo vya nyumbani na viwanda vidogo vya usindikaji na utengenezaji bidhaa. Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 ililenga kufanya mageuzi kutoka uchumi unaotegemea kilimo kuwa uchumi wa kati unaotegemea viwanda, kwa kutilia mkazo shughuli za kilimo, viwanda, ufugaji, na uvuvi na hivyo kufanya mageuzi ya kiuchumi vijijini na kuleta maendeleo ya taifa kwa ujumla.

Katika jitihada za kuimarisha na kuendeleza viwanda vijijini, Serikali ilichukua hatua mbalimbali ukiwamo ujenzi na upanuzi wa barabara na usambazaji wa maji katika maeneo mengi ya vijijini. Aidha, Serikali ilianzisha Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) na Idara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika halmashauri zote nchini ili kusaidia kuleta maendeleo vijijini na mageuzi ya viwanda.

Vilevile, utekelezaji wa programu mbalimbali umeleta tija katika kufanikisha mpango wa uendelezaji wa viwanda vijijini. Mojawapo ya programu hizo ni Muunganisho Ujasiriamali Vijijini (MUVI) uliotekelezwa na Serikali kuanzia mwaka 2008 hadi 2016, ambao ulisaidia kuimarisha ujasiriamali vijijini kwa kuwawezesha wakazi wa vijijini kuanzisha biashara za mazao maalumu kwa kuzingatia mnyororo wa thamani. Mradi huu ulitekelezwa katika mikoa ya Iringa, Njombe, Manyara, Mwanza, Pwani, Ruvuma na Tanga.

Programu nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa Miundombinu ya Masoko; Uongezaji Thamani wa Mazao na Uboreshaji wa Huduma za Kifedha Vijijini (MIVARF). Programu hizo ziliwawezesha wakulima wadogo kuunda vikundi vya kiuchumi vilivyosaidia wanachama kupata rasilimali fedha, teknolojia mpya na ujuzi uliowawesha kuongeza tija na kuboresha bidhaa zao, pamoja na kupata masoko endelevu ya bidhaa hizo. Programu hizo zilitekelezwa katika mikoa 26, ikijumuisha mikoa 21 ya Tanzania Bara na mikoa mitano (5) ya Zanzibar, ikihusisha wilaya 141 za vijijini. Aidha, Ushoroba wa Ukuzaji Kilimo Tanzania (AGCOT), ambao unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi, umechangia ongezeko la mapato na ajira kupitia uendelezaji wa mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania. Mpango huo ulilenga kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, kuendeleza miundombinu wezeshi pamoja na kuongeza uzalishaji wenye tija.

Jitihada nyingine zilizofanywa na Serikali kupitia Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC) ni pamoja na kuandaa chasili za awali za mashine mbalimbali za kilimo na teknolojia za vijijini kama vile teknolojia za maandalizi ya ardhi kwa ajili kilimo (modeli 2), teknolojia za upandaji mbegu (modeli 2), teknolojia ya usafirishaji wa mazao vijijini (modeli 1), teknolojia za usindikaji wa mazao ya kilimo (modeli 4) na teknolojia za kuwasha na kuzima moto katika hifadhi za wanyamapori (modeli 3). Aidha, kituo hicho kilitoa mafunzo kwa vijana 520 waliopo maeneo ya vijijini kuhusu kubuni teknolojia za nishati jadidifu kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa nishati safi ya kupikia. Kupitia mafunzo hayo mitambo mikubwa mitano (5) ya biogesi ilijengwa.

Hata hivyo, kasi ya uendelezaji wa viwanda vijijini bado ni ndogo kutokana na changamoto kadhaa kama vile ukosefu wa elimu na ujuzi wa uendeshaji wa viwanda; kukosekana kwa maofisa ugani wa viwanda vijijini; na miundombinu duni ya kusaidia maendeleo ya viwanda vijijini.

2.1.8. Uendelezaji Jasiriamali

Uendelezaji jasiriamali katika muktadha wa sera hii unahusisha ukuzaji, uanzishwaji na uendelezaji biashara changa na urasimishaji wa biashara. Ukuaji wa biashara ni kichocheo muhimu katika kuleta ushindani wa kiuchumi na kuongeza ajira. Ukuaji huu hupimwa kwa vigezo mbalimbali kama vile mauzo au mapato, idadi ya wafanyakazi, mali, kiwango cha mauzo katika soko, faida, uwezo wa uzalishaji na mtaji wa uwekezaji.

Sera ya Maendeleo ya Jasiriamali Ndogo na Kati ya mwaka 2003 ililenga kuhamasisha shughuli za ujasiriamali miongoni mwa Watanzania. Lengo hilo limefanikiwa kwa kiwango cha kuridhisha kwa kuanzisha mafunzo ya ujasiriamali katika taasisi za elimu ya juu na vyuo vya kati, kubuni programu maalumu za kuwawezesha wajasiriamali, na kujumuisha elimu ya ujasiriamali katika mitaala ya shule za msingi na sekondari. Mafanikio ya mafunzo ya ujasiriamali yanajidhihirisha kwa kuongezeka kwa idadi ya wajasiriamali kutoka milioni 1.5 mwaka 2003 hadi kufikia milioni 8 mwaka 2020.

Licha ya ongezeko la idadi ya jasiriamali, kasi ya ukuaji wake bado ni ndogo na hivyo kuwa na mchango mdogo katika ajira na uchumi wa taifa. Mathalani, watu milioni 8 walioajiriwa katika biashara milioni 4.5 huchangia wastani wa nafasi 1.7 za ajira kwa kila biashara. Kutokana na hali hiyo juhudi madhubuti zinahitajika ili kuimarisha uendelezaji jasiriamali na kuhamasisha urasimishaji wa biashara ndogo na za kati, kuendeleza biashara changa na kuongeza mchango wa biashara ndogo na za kati katika ajira na uchumi wa taifa.

Aidha, kuna fursa mpya ambazo bado hazijatumika kikamilifu katika sekta za uchimbaji wa rasilimali na ubunifu kwa ajili ya biashara ndogo na za kati. Sekta ya uchimbaji wa rasilimali inahusisha michakato ya shughuli zinazolenga uchimbaji wa malighafi za ardhini (kama vile mafuta, metali, madini na kokoto), usindikaji na matumizi yake kwa walaji. Katika sekta ya mafuta na gesi, shughuli za uchimbaji zimegawanyika katika sehemu kuu tatu: mkondo wa juu wa uchimbaji (utafiti, uendelezaji na uzalishaji), mkondo wa kati wa uchimbaji (usafirishaji na uhifadhi) na mkondo wa chini wa uchimbaji (utengenezaji wa bidhaa, usindikaji wa gesi na uuzaji wa bidhaa). Katika sekta ya madini, shughuli kuu zimegawanyika katika uchimbaji (utafiti, uendelezaji na uchimbaji) na uchenjuaji (usafishaji, uongezaji thamani, usafirishaji na uhifadhi).

Vilevile, sekta ya ubunifu inajumuisha shughuli mbalimbali kama vile ubunifu wa mitindo, muziki, uchapishaji, usanifu majengo, filamu na video, ufundi wa mikono, sanaa za uchoraji, mitindo ya mavazi, televisheni na redio, matangazo, fasihi, michezo ya kompyuta, na sanaa za maonesho.

Sekta hizi mbili zinatoa fursa kubwa kwa biashara ndogo na za kati. Ujumuishaji wa sekta za uchimbaji wa rasilimali na ubunifu katika sera hii utasaidia wadau kunufaika na fursa zilizopo katika sekta hizo.

2.1.9. Masuala Mtambuka

Sera ya Maendeleo ya Jasiriamali Ndogo na Kati ya mwaka 2003 ilitambua athari za kimazingira zinazotokana na shughuli mbalimbali za wajasiriamali wadogo na wa kati na ilibainisha umuhimu wa kuzingatia matakwa ya kanuni za mazingira kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati. Ili kupunguza changamoto hizo, Serikali ilichukua hatua kadhaa ikiwa ni pamoja na kutunga Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (EMA, 2004) ambayo inaweka utaratibu wa kisheria na kitaasisi wa usimamizi endelevu wa mazingira.

Hatua nyingine zilizochukuliwa na Serikali ni kuandaa mikakati na mipango mbalimbali ikiwamo Mkakati wa Hatua za Dharura kwa Uharibifu wa Ardhi na Vyanzo vya Maji (2006); Mkakati wa Kitaifa wa Hatua za Dharura za Uhifadhi wa Ukanda wa Pwani, Bahari, Maziwa, Mito na Mabwawa (2008); Mkakati wa Kitaifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (2012); na Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 – 2032). Aidha, Serikali imeridhia mikakati mbalimbali ya kikanda na kimataifa inayohusu masuala ya mazingira.

Aidha, Serikali ilitoa upendeleo kwa baadhi ya mahitaji ya kisheria kwa wafanyabishara wadogo na wa kati kuhusu utunzaji wa mazingira na kutoa mafunzo ya uhifadhi wa mazingira. Pamoja na hatua hizo zilizochukuliwa na Serikali, bado kuna changamoto ya wafanyabishara wadogo na wa kati kutozingatia utunzaji wa mazingira. Changamoto hizo zinatokana na sababu mbalimbali ikiwamo masuala ya mazingira kutojumuishwa kikamilifu katika shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira. Sera hii imezingatia umuhimu wa kujumuisha masuala ya mazingira katika shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati.

Janga la VVU na UKIMWI linaendelea kuwa tishio kwa afya ya Watanzania kwa ujumla, hususan kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati kwa kuathiri uzalishaji, nguvukazi na uendelezaji ujuzi. Mwaka 2001, Serikali ilitunga na kutekeleza Sera ya Taifa ya UKIMWI ya mwaka 2001 na Sheria ya kuanzisha Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) 2001 ili kuimarisha mapambano dhidi ya maambukizi, kutoa huduma za matibabu, na kuweka mazingira wezeshi ya kupunguza maambukizi ya VVU. Hatua hizo zimesaidia kuongeza uelewa na kupunguza maambukizi ya VVU na UKIMWI.

Takwimu za TACAIDS za mwaka 2019 zinaonesha kuwa asilimia 83 ya watu wanaoishi na VVU walikuwa wanajua hali zao; asilimia 98 walikuwa kwenye matibabu; asilimia 92 walikuwa na kiwango cha chini cha virusi mwilini; asilimia 92 ya watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi waliokuwa na VVU walikuwa kwenye matibabu; na asilimia 99 ya wanawake wajawazito waliokuwa na VVU walipata dawa za kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Vilevile, Serikali imeendelea kushirikiana na sekta binafsi, Washirika wa Maendeleo na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kutekeleza afua za kijamii dhidi ya VVU na UKIMWI.

Sekta ya Maendeleo ya Jasiriamali Ndogo na Kati inahusisha mwingiliano wa watu mbalimbali katika shughuli za kila siku, hali inayoongeza hatari ya maambukizi ya VVU na UKIMWI. Aidha, baadhi ya shughuli za wafanyabiashara wadogo na wa kati zinaweza kuwa chanzo cha magonjwa yasiyoambukizwa (NCDs) ambayo huwafanya waathirika wahitaji msaada wa kijamii na kisaikolojia. Hata hivyo, masuala ya VVU, UKIMWI na magonjwa yasiyoambukizwa hayajazingatiwa ipasavyo katika shughuli za wafanyabiashara wadogo na wa kati kutokana na uelewa mdogo wa wajasiriamali juu ya hatua za kujikinga na kujiepusha na changamoto hizo za kiafya.

Sera hii imezingatia umuhimu wa kutilia mkazo ujumuishaji wa masuala ya VVU, UKIMWI na magonjwa yasiyoambukizwa katika shughuli za wafanyabiashara wadogo na wa kati.

Kwa upande wa masuala ya usawa wa kijinsia, Serikali imeweka mifumo ya kisera na kisheria inayowezesha ushiriki wa wanawake katika uchumi kupitia Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000, toleo la mwaka 2023, na Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Jinsia (NGDS) wa mwaka 2005. Hatua hizo zimewezesha ujumuishwaji wa masuala ya usawa wa kijinsia katika shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi, hali ambayo imehamasisha wanawake kuanzisha, kusimamia na kukuza biashara zao.

Aidha, Serikali ilifanya marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura ya 290, ambayo inazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga asilimia 10 ya mapato yao ya ndani kwa ajili ya kuwawezesha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Hatua hiyo imeongeza idadi ya wanawake wanaofanya biashara ndogo na za kati kushiriki katika shughuli za kiuchumi. Vijana, hususan wanawake, wanawakilisha kundi kubwa la idadi ya watu nchini. Hata hivyo, wengi wao wanajihusisha na biashara ndogo na za kati katika sekta isiyo rasmi. Hii inatokana na changamoto za upatikanaji wa rasilimali kwa usawa, mila na desturi potofu za kijamii, ukosefu wa ujuzi wa kutosha na changamoto ya upatikanaji wa masoko ya bidhaa na huduma mbalimbali.

Ili kuongeza ushiriki wa vijana katika shughuli za kiuchumi na ujasiriamali, Serikali iliandaa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007 toleo la mwaka 2024. Vilevile, Serikali imeendelea kufadhili Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, unaotoa mikopo nafuu kwa vijana. Hatua hizo zinalenga kukuza shughuli za ujasiriamali miongoni mwa vijana katika sekta isiyo rasmi, kuwasaidia kujiajiri na kupunguza ukosefu wa ajira kwa vijana. Mafanikio mengine ni pamoja na kuanzisha na kutekeleza Programu za Mafunzo ya Uanagenzi kwa Vijana na Programu ya Taifa ya Kukuza na Kuendeleza Ujuzi, ambayo imeongeza uwezo wa vijana.

Licha ya jitihada mbalimbali zilizofanyika, ukosefu wa ajira kwa vijana umeendelea kuwa changamoto, hasa maeneo ya vijijini. Ushiriki wa vijana katika biashara rasmi pia ni mdogo kutokana na ukosefu wa mitaji hasa kwa biashara changa, na kutokulingana kwa ujuzi miongoni mwao na mahitaji ya soko. Hadi kufikia mwaka 2020/2021, idadi ya vijana nchini Tanzania ilikuwa milioni 18.28, ambapo milioni 17.71 walikuwa Tanzania Bara na milioni 0.57 walikuwa Zanzibar. Katika idadi hiyo, takriban vijana milioni 14.62 (80%) walikuwa wanashiriki katika shughuli za kiuchumi, huku vijana milioni 3.66 (20%) wakiwa hawashiriki katika shughuli za kiuchumi.

Miongoni mwa vijana waliokuwa wanashiriki katika shughuli za kiuchumi, milioni 12.78 (87.4%) walikuwa wameajiriwa, na milioni 1.84 (12.6%) walikuwa hawana ajira. Vijana wengi (62.4%) walijishughulisha na kilimo, bidhaa za misitu na uvuvi, 12.6% walijihusisha na biashara ya rejareja na ufundi magari, huku 5.1% wakijihusisha na utengenezaji wa bidhaa viwandani.

Sera ya Maendeleo ya Jasiriamali Ndogo na Kati, (Toleo la mwaka 2025) inatambua fursa na changamoto zinazolikabili kundi la vijana na inasisitiza haja ya Serikali kubuni mikakati inayolenga kusaidia shughuli za biashara ndogo na za kati kwa kuzingatia mahitaji na matarajio maalumu ya vijana.

2.2. Umuhimu wa kufanya marekebisho

Licha ya mafanikio yaliyopatikana kupitia Sera ya Maendeleo ya Jasiriamali Ndogo na Kati ya Mwaka 2003, Jasiriamali Ndogo na za Kati ziliendelea kukabiliwa na changamoto nyingi zilizohitaji marekebisho ya sera hiyo. Changamoto hizo ni kuibuka kwa fursa mpya katika sekta kama vile matumizi ya TEHAMA katika shughuli za kibiashara na kukua kwa tasnia ya ubunifu hazikuzingatiwa katika sera hiyo.

Vilevile, kuongezeka kwa shughuli za soko huria hususan ushiriki wa sekta binafsi katika maendeleo ya jasiriamali ndogo na za kati, kulihitaji mwongozo wa kisera. Aidha, matumizi ya vigezo vya idadi ya wafanyakazi na ukubwa wa mitaji iliyowekezwa katika mitambo kubainisha madaraja ya biashara, ambapo mabadiliko katika viashiria vya uchumi jumla yalilazimu haja ya kupanga upya vigezo hivyo. Kadhalika, makubaliano ya mtangamano wa biashara wa kikanda na kimataifa yanayozitaka nchi wanachama kuoanisha sera yalipaswa kuzingatiwa. Pamoja na hayo mahitaji ya biashara changa zinazokua kwa kasi yalihitaji mwongozo wa kisera. Zaidi hayo, mwongozo wa Serikali wa uandaaji wa sera ulipaswa kuzingatiwa katika toleo jipya la sera.

SURA YA TATU

3. DIRA, DHAMIRA NA MALENGO

3.1.Dira na Dhamira

3.1.1. Dira

Kuwa na sekta imara na himilivu ya jasiriamali ndogo na za kati ambayo inachangia kikamilifu katika maendeleo ya uchumi.

3.1.2. Dhamira

Kuchochea maendeleo na ukuaji wa jasiriamali ndogo na za kati kwa kuboresha miundombinu ya biashara; kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji rahisi wa fedha na masoko; na kuhimiza matumizi ya teknolojia na ubunifu katika ukuzaji wa biashara.

3.2. Malengo ya Sera

3.2.1. Lengo Kuu

Kuchochea ajira na ukuzaji wa kipato kwa kuhamasisha uanzishaji wa jasiriamali mpya ndogo na za kati na kuboresha utendaji kazi na ushindani wa zile zilizopo ili kuongeza ushiriki na mchango wao katika uchumi wa nchi.

3.2.2. Malengo Mahususi

(i) Kuimarisha miundombinu wezeshi ya shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati;
(ii) Kuimarisha ukuaji wa jasiriamali ndogo na za kati mijini na vijijini;
(iii) Kuongeza matumizi ya teknolojia na ubunifu kwa wajasiriamali wadogo na wa kati;
(iv) Kuwezesha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wajasiriamali wadogo na wa kati;
(v) Kuwezesha upatikanaji wa masoko ya bidhaa na huduma zinazozalishwa na wajasiriamali wadogo na wa kati; na
(vi) Kujumuisha masuala mtambuka katika shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati.

SURA YA NNE

4. MALENGO, MIKAKATI NA SHABAHA

4.1. Miundombinu Wezeshi

Lengo

Kuimarisha miundombinu wezeshi ya shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati.

Mikakati

i. Kuwezesha upatikanaji wa maeneo kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza jasiriamali ndogo na za kati ;
ii. Kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha na kuendeleza miundombinu kwa ajili ya wajasiriamali wadogo na wa kati; na
iii. Kuanzisha na kuimarisha kongani za viwanda kwa ajili ya wajasiriamali wadogo na wa kati.

Shabaha

i. Kuongezeka kwa majengo ya viwanda kwa ajili wajasiriamali wadogo na wa kati kutoka 467 hadi kufikia 654 ifikapo Juni 2035;
ii. Kuongezeka kwa maghala ya kuhifadhia bidhaa za wajasiriamali wadogo na wa kati kutoka maghala 328 hadi 1,000 ifikapo Juni 2035;
iii. Kuongezeka kwa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati kutoka mita za mraba bilioni 6.25 hadi kufikia bilioni 12.49 ifikapo Juni 2035; na
iv. Kuongezeka kwa kongani za viwanda kwa ajili ya shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati kutoka 57 hadi kufikia 114 ifikapo Juni 2035.

Viashiria vya Matokeo

Badiliko la idadi ya wajasiriamali wadogo na wa kati.

4.2. Uendelezaji Jasiriamali

Lengo

Kuimarisha ukuaji wa jasiriamali ndogo na za kati mijini na vijijini.

Mikakati

i. Kuhamasisha urasimishaji biashara, uendelezaji biashara changa na ukuaji wa jasiriamali;
ii. Kuwezesha uanzishaji na uimarishaji wa vituo atamizi vya biashara kwa ajili ya wajasiriamali wadogo na wa kati katika Serikali za Mitaa na taasisi za mafunzo;
iii. Kuwezesha wajasiriamali wadogo na wa kati kutumia fursa zinazoibuka katika sekta zote; na
iv. Kujenga uwezo wa usimamizi na uendeshaji biashara kwa wajasiriamali wadogo na wa kati.

Shabaha

i. Kuongezeka kwa idadi ya wajasiriamali wadogo na wa kati waliopata mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara kutoka 69,536 hadi kufikia 229,532 ifikapo Juni 2035;
ii. Kuongezeka kwa biashara rasmi kutoka16,489 mwaka 2024 hadi kufikia 80,000 mwaka Juni 2035;
iii. Kuongezeka kwa vituo atamizi vya wajasiriamali wadogo na wa kati kutoka 6 hadi kufikia 26 ifikapo Juni 2035;
iv. Kuandaliwa na kutumika kwa mwongozo wa urasimishaji biashara ifikapo Juni 2027; na
v. Kuhuishwa na kutumika kwa mwongozo wa mafunzo ya ujasiriamali kwa wajasiriamali wadogo na wa kati ifikapo Juni 2027.

Viashiria vya Matokeo

i. Badiliko la kiwango cha jasiriamali ndogo na za kati zinazofungwa kwa mwaka; na
ii. Badiliko la idadi ya jasiriamali ndogo na za kati zilizosajiliwa.

4.3. Teknolojia na Ubunifu

Lengo

Kuongeza matumizi ya teknolojia na ubunifu kwa wajasiriamali wadogo na wa kati.

Mikakati

i. Kuimarisha taasisi za utafiti ili kuharakisha maendeleo ya jasiriamali ndogo na za kati;
ii. Kuimarisha upatikanaji wa miundombinu ya TEHAMA kwa ajili ya wajasiriamali wadogo na wa kati; na
iii. Kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika shughuli za jasiriamali ndogo na za kati.

Shabaha

i. Kuongezeka kwa idadi ya vituo vya kuendeleza teknolojia kutoka 7 hadi kufikia 26 ifikapo Juni 2035;
ii. Kuongezeka kwa idadi ya mitambo inayotengenezwa kwa mwaka kwa ajili ya wajasiriamali wadogo na wa kati kutoka 493 hadi kufikia 986 ifikapo Juni 2035;
iii. Kuongezeka kwa idadi ya vipuri vinavyotengezwa kwa mwaka kwa ajili ya wajasiriamali wadogo na wa kati ifikapo Juni 2035;
iv. Kuongezeka kwa ubunifu wa teknolojia kwa mwaka kwa ajili ya maendeleo ya jasiriamali ndogo na za kati kutoka 3 hadi kufikia 6 ifikapo Juni 2035; na
v. Kuongezeka kwa matumizi ya TEHAMA katika shughuli za jasiriamali ndogo na za kati ifikapo Juni 2035.

Viashiria vya Matokeo

i. Badiliko la ubora na aina za bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali wadogo na wa kati; na
ii. Badiliko la idadi ya jasiriamali ndogo na za kati zinazotumia biashara-mtandao.

4.4. Upatikanaji wa Huduma za Kifedha

Lengo

Kuwezesha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wajasiriamali wadogo na wa kati.

Mikakati

i. Kujenga uwezo wa ujuzi wa kupata mitaji kwa wajasiriamali wadogo na wa kati;
ii. Kuimarisha uhusiano baina ya jasiriamali ndogo na za kati na taasisi za kifedha; na
iii. Kuhamasisha na kuwezesha upatikanaji wa mitaji ya kuendeleza biashara changa.

Shabaha

i. Kuongezeka kwa mikopo inayotolewa kwa wajasirimali wadogo na wa kati kutoka shilingi bilion 945.7 hadi kufikia shilingi trilioni 4.7 ifikapo Juni 2035;
ii. Jasiriamali milioni 5 kuunganishwa na taasisi za kifedha ifikapo Juni 2035; na
iii. Biashara changa milioni 1 kupata mitaji kutoka kwenye taasisi za fedha ifikapo Juni 2035.

Viashiria vya Matokeo

Kiwango cha upatikanaji wa huduma za mitaji kwa wajasiriamali wadogo na wa kati.

4.5. Upatikanaji wa Masoko

Lengo

Kuwezesha upatikanaji wa masoko ya bidhaa na huduma zinazozalishwa na wajasiriamali wadogo na wa kati.

Mikakati

i. Kuwezesha programu za kujenga uwezo kwa wajasirimali wadogo na wa kati kuhusu upatikanaji wa masoko ya kitaifa, kikanda na kimataifa;
ii. Kuimarisha uhusiano baina ya wajasiriamali wadogo na wa kati na kampuni kubwa;
iii. Kuwaunganisha wajasiriamali wadogo na wa kati na wafanyabiashara wakubwa;
iv. Kuhamasisha wajasiriamali wadogo na wa kati kufanya shughuli zao katika vikundi na vyama vya ushirika; na
v. Kuimarisha taasisi za utafutaji masoko zinazosaidia jasiriamali ndogo na za kati.

Shabaha

i. Kuongezeka kwa idadi ya wajasiriamali wadogo na wa kati wanaoshiriki maonesho ya ndani kwa mwaka kutoka 1,379 hadi kufikia 6,899 ifikapo Juni 2035;
ii. Kuongezeka kwa idadi ya wajasiriamali wadogo na wa kati wanaoshiriki masoko ya kimataifa kwa mwaka kutoka 625 hadi kufikia 3,123 ifikapo Juni 2035;
iii. Kuzijengea uwezo taasisi tatu (3) za masoko zinazowezesha jasiriamali ndogo na za kati ifikapo Juni 2035;
iv. Kuunganisha jasiriamali ndogo na za kati 1,900,000 na kampuni kubwa za ndani ifikapo Juni 2035;
v. Kuunganisha jasiriamali ndogo na za kati 500,000 na kampuni kubwa za nje ifikapo Juni 2035; na
vi. Jasirimali ndogo na za kati 3,000,000 kupata mafunzo ya utafutaji wa masoko ifikapo Juni 2035.

Viashiria vya Matokeo

Badiliko la kiwango cha mauzo katika soko kwa bidhaa zilizozalishwa na jasiriamali ndogo na za kati katika soko la kitaifa, kikanda na kimataifa.

4.6. Masuala Mtambuka

Lengo

Kujumuisha masuala mtambuka katika shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati.

Mikakati

i. Kujenga uelewa wa masuala ya mazingira na fursa zilizopo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati;
ii. Kuwezesha upatikanaji na matumizi ya teknolojia rafiki za mazingira kwa wajasiriamali wadogo na wa kati;
iii. Kuhamasisha ushiriki wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika shughuli za ujasiriamali;
iv. Kuhamasisha ujumuishaji wa masuala ya VVU/UKIMWI na magonjwa yasiyoambukizwa katika shughuli za ujasiriamali; na
v. Kuhamasisha ujumuishaji wa masuala ya utawala bora katika shughuli za ujasiriamali.

Shabaha

i. Jasiriamali 6,000,000 kupata uelewa wa hatua za kulinda mazingira ifikapo Juni, 2035;
ii. Jasiriamali 1,500,000 kutumia teknolojia rafiki za mazingira ifikapo Juni 2035;
iii. Wanawake wajasiriamali 1,000,000 kupata mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara ifikapo Juni 2035;
iv. Vijana wajasiriamali 3,500,000 kupata mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara ifikapo Juni 2035;
v. Wajasiriamali wenye ulemavu 500,000 kupata mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara ifikapo Juni 2035;
vi. Wanawake wajasiriamali 1,000,000 kupata huduma za kifedha ifikapo Juni 2035;
vii. Vijana wajasiriamali 3,500,000 kupata huduma za kifedha ifikapo Juni 2035;
viii. Wajasiriamali wenye ulemavu 500,000 kupata huduma za kifedha ifikapo Juni 2035;
ix. Wajasiriamali 3,000,000 kupata uelewa kuhusu VVU/UKIMWI ifikapo Juni 2035;
x. Wajasiriamali 1,000,000 kupata uelewa kuhusu magonjwa yasiyoambukizwa ifikapo Juni 2035.

Viashiria vya Matokeo

i. Kiwango cha wajasiriamali kuzingatia utunzaji wa mazingira;
ii. Badiliko la idadi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wanaojihusisha na shughuli za ujasiriamali; na
iii. Badiliko la kiwango cha watu wenye VVU/UKIMWI na magonjwa yasiyoambukizwa kwa wajasiriamali.

SURA YA TANO

5. MPANGO WA UTEKELEZAJI

5.1. Utangulizi

Mpango wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jasiriamali Ndogo na za Kati ya mwaka 2003 (Toleo la mwaka 2025) umebainisha rasilimali, muda, na wadau wa utekelezaji kama inavyofafanuliwa katika vipengele vifuatavyo.

5.2. Rasilimali Fedha

Jumla ya shilingi za Kitanzania trilioni 1.79 zitatumika kuwezesha utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jasiriamali Ndogo na za Kati ya mwaka 2003 (Toleo la mwaka 2025). Fedha hizo zitatolewa na serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi; washirika wa maendeleo; na wadau wengine.

5.3. Muda wa Utekelezaji

Mkakati huu utatekelezwa katika kipindi cha miaka 10 kuanzia mwaka 2025 hadi mwaka 2035. Muda huo umebainishwa kwenye bangokitita la mpango wa utekelezaji katika Jedwali Na. 1.

Jedwali Na. 1: Bangokitita la Mpango wa Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jasiriamali Ndogo na za Kati ya Mwaka 2003 (Toleo la mwaka 2025)Ii

Na	Malengo	Mikakati	Shabaha	Muda	Rasilimali Fedha (Shs. Mil)	Watekelezaji
1	Kuimarisha miundombinu wezeshi ya shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati.	Kuwezesha upatikanaji wa maeneo kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza jasiriamali ndogo na za kati.	Kuongezeka kwa majengo ya viwanda kwa ajili wajasiriamali wadogo na wa kati kutoka 467 hadi kufikia 654 ifikapo Juni 2035.	2035	**187,000**	**WVB** MoF, SIDO, NEEC, POPI, TAMISEMI, MoW, MoT, MoICT TPSF, Washirika wa Maendeleo na Taasisi zingine za Umma.
			Kuongezeka kwa maghala ya kuhifadhia bidhaa za wajasiriamali wadogo na wa kati kutoka maghala 328 hadi 1,000 ifikapo Juni 2035.	2035	**210,000**	**WVB** MoF, SIDO, NEEC, POPI, TAMISEMI, MoW, MoT, MoICT TPSF, Washirika wa Maendeleo na Taasisi zingine za Umma.
			Kuongezeka kwa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati kutoka mita za mraba bilioni 6.25 hadi kufikia bilioni 12.49 ifikapo Juni 2035.	2035	**540,000**	**WVB** MoF, SIDO, NEEC, POPI, TAMISEMI, MoW, MoT, MoICT TPSF, Washirika wa Maendeleo na Taasisi zingine za Umma.
		Kuanzisha na kuimarisha kongani za viwanda kwa ajili ya wajasiriamali wadogo na wa kati.	Moduli za mafunzo ya ujuzi maalumu katika uongezaji thamani kujumuishwa katika mitaala ya ufundi stadi ifikapo Juni 2027 Kuongezeka kwa kongani za viwanda kwa ajili ya shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati kutoka 57 hadi kufikia 114 ifikapo Juni 2035.	2035	**250,000**	**WVB** MoF, SIDO, NEEC, POPI, TAMISEMI, MoW, MoT, MoICT TPSF, Washirika wa Maendeleo na Taasisi zingine za Umma.

Na	Malengo	Mikakati	Shabaha	Muda	Rasilimali Fedha (Shs. Mil)	Watekelezaji
2	Kuimarisha ukuaji wa jasiriamali ndogo na za kati mijini na vijijini	Kuhamasisha urasimishaji biashara, uendelezaji biashara changa na ukuaji wa jasiriamali	Kuongezeka kwa biashara rasmi kutoka 16,489 mwaka 2024 hadi kufikia 80,000 mwaka Juni 2035.	2035	**10,000**	**WVB** MoF, TAMISEMI, SIDO, COSTECH, TIRDO, NEEC, TPSF, CAMARTEC, TEMDO, Taasisi za utafiti na Elimu, Washirika wa Maendeleo na Taasisi zingine za Umma.
			Kuandaliwa na kutumika kwa mwongozo wa urasimishaji biashara ifikapo Juni 2027.	2027	**2,000**	**WVB** MoF, TAMISEMI, SIDO, NEEC, TPSF, Washirika wa Maendeleo na Taasisi zingine za Umma.
		Kuwezesha uanzishaji na uimarishaji wa vituo atamizi vya wajasiriamali wadogo na wa kati katika serikali za mitaa na taasisi za mafunzo.	Kuongezeka kwa vituo atamizi vya wajasiriamali wadogo na wa kati kutoka 6 hadi kufikia 26 ifikapo Juni 2035.	2035	**355,000**	**WVB** MoF, TAMISEMI, SIDO, NEEC, TPSF, Washirika wa Maendeleo na Taasisi zingine za Umma.
		Kujenga uwezo wa usimamizi na uendeshaji biashara kwa wajasiriamali wadogo na wa kati	Kuongezeka kwa idadi ya wajasiriamali wadogo na wa kati waliopata mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara kutoka 69,536 hadi kufikia 229,532 ifikapo Juni 2035.	2035	**8,000**	**WVB** MoF, TAMISEMI, SIDO, COSTECH, TIRDO, NEEC, TPSF, CAMARTEC, TEMDO, Taasisi za utafiti na Elimu, Washirika wa Maendeleo na Taasisi zingine za Umma.
		Kuhuishwa na kutumika kwa mwongozo wa mafunzo ya ujasiriamali kwa wajasiriamali wadogo na wa kati ifikapo Juni 2027.		2027	**2,000**	**WVB** MoF, TAMISEMI, SIDO, COSTECH, TIRDO, NEEC, TPSF, CAMARTEC, TEMDO, Taasisi za utafiti na Elimu, Washirika wa Maendeleo na Taasisi zingine za Umma.

Na	Malengo	Mikakati	Shabaha	Muda	Rasilimali Fedha (Shs. Mil)	Watekelezaji
3	Kuongeza matumizi ya teknolojia na ubunifu kwa wajasiriamali wadogo na wa kati.	Kuimarisha taasisi za utafiti ili kuharakisha maendeleo ya jasiriamali ndogo na za kati.	Kuongezeka kwa idadi ya vituo vya kuendeleza teknolojia kutoka 7 hadi kufikia 26 ifikapo Juni 2035.	2035	**65,000**	**WVB** MoF, TAMISEMI, SIDO, COSTECH, TIRDO, NEEC, TPSF, CAMARTEC, TEMDO, Taasisi za utafiti na Elimu, Washirika wa Maendeleo na Taasisi zingine za Umma.
			Kuongezeka kwa idadi ya mitambo inayotengenezwa kwa mwaka kwa ajili ya wajasiriamali wadogo na wa kati kutoka 493 hadi kufikia 986 ifikapo Juni 2035.	2035	**9,000**	**WVB** MoF, TAMISEMI, SIDO, COSTECH, TIRDO, NEEC, TPSF, CAMARTEC, TEMDO, Taasisi za utafiti na Elimu, Washirika wa Maendeleo na Taasisi zingine za Umma.
			Kuongezeka kwa idadi ya vipuri vinavyotengezwa kwa mwaka kwa ajili ya wajasiriamali wadogo na wa kati ifikapo Juni 2035.	2035	**11,000**	**WVB** MoF, TAMISEMI, SIDO, COSTECH, TIRDO, NEEC, TPSF, CAMARTEC, TEMDO, Taasisi za utafiti na Elimu, Washirika wa Maendeleo na Taasisi zingine za Umma.
			Kuongezeka kwa ubunifu wa teknolojia kwa mwaka kwa ajili ya maendeleo ya jasiriamali ndogo na za kati kutoka 3 hadi kufikia 6 ifikapo Juni 2035.	2035	**25,000**	**WVB** MoF, TAMISEMI, SIDO, COSTECH, TIRDO, NEEC, TPSF, CAMARTEC, TEMDO, Taasisi za utafiti na Elimu, Washirika wa Maendeleo na Taasisi zingine za Umma.
		Kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika shughuli za jasiriamali ndogo na za kati.	Kuongezeka kwa matumizi ya TEHAMA katika shughuli za jasiriamali ndogo na za kati ifikapo Juni 2035.	2035	**10,000**	**WVB** MoF, TAMISEMI, SIDO, COSTECH, TIRDO, NEEC, TPSF, CAMARTEC, TEMDO, Taasisi za utafiti na Elimu, Washirika wa Maendeleo na Taasisi zingine za Umma.

Na	Malengo	Mikakati	Shabaha	Muda	Rasilimali Fedha (Shs. Mil)	Watekelezaji
4	Kuwezesha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wajasiri-amali wadogo na wa kati.	Kujenga uwezo wa ujuzi wa kupata mitaji kwa wajasiriamali wadogo na wa kati.	Kuongezeka kwa mikopo inayotolewa kwa wajasiriamali wadogo na wa kati kutoka shilingi bilion 945.7 hadi kufikia shilingi trilioni 4.7 ifikapo Juni 2035.	2035	**9,000**	**WVB** MoF, TAMISEMI, SIDO, COSTECH, TIRDO, NEEC, TPSF, CAMARTEC, TEMDO, Taasisi za utafiti na Elimu, Washirika wa Maendeleo na Taasisi zingine za Umma.
		Kuimarisha uhusiano baina ya jasiriamali ndogo na za kati na taasisi za kifedha.	Jasiriamali milioni 5 kuunganishwa na taasisi za kifedha ifikapo Juni, 2035.	2035	**5,500**	**WVB** MoF, TAMISEMI, SIDO, COSTECH, TIRDO, NEEC, TPSF, CAMARTEC, TEMDO, Taasisi za utafiti na Elimu, Washirika wa Maendeleo na Taasisi zingine za Umma.
		Kuhamasisha na kuwezesha upatikanaji wa mitaji ya kuendeleza biashara changa.	Biashara changa milioni 1 kupata mitaji kutoka kwenye taasisi za fedha ifikapo Juni 2035.	2035	**5,000**	**WVB** MoF, TAMISEMI, SIDO, COSTECH, TIRDO, NEEC, TPSF, CAMARTEC, TEMDO, Taasisi za utafiti na Elimu, Washirika wa Maendeleo na Taasisi zingine za Umma.
5	Kuwezesha upatikanaji wa masoko ya bidhaa na huduma zinazalishwa na wajasiria-mali wadogo na wa kati.	Kuwezesha programu za kujenga uwezo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati kuhusu upatikanaji wa masoko ya kitaifa, kikanda na kimataifa	Kuongezeka kwa idadi ya wajasiria-mali wadogo na wa kati wanaoshiriki maonesho ya ndani kwa mwaka kuto-ka 1,379 hadi kufikia 6,899 ifikapo Juni 2035.	2035	**10,500**	**WVB** MoF, TAMISEMI, SIDO, COSTECH, TIRDO, NEEC, TPSF, CAMARTEC, TEMDO, Taasisi za utafiti na Elimu, Washirika wa Maendeleo na Taasisi zingine za Umma.

Na	Malengo	Mikakati	Shabaha	Muda	Rasilimali Fedha (Shs. Mil)	Watekelezaji
			Kuongezeka kwa idadi ya wajasiria-mali wadogo na wa kati wanaoshiriki masoko ya kimataifa kwa mwaka ku-toka 625 hadi kufikia 3,123 ifikapo Juni 2035.	2035	**16,500**	**WVB** MoF, TAMISEMI, SIDO, COSTECH, TIRDO, NEEC, TPSF, CAMARTEC, TEMDO, Taasisi za utafiti na Elimu, Washirika wa Maendeleo na Taasisi zingine za Umma.
			Jasirimali ndogo na za kati 3,000,000 kupata mafunzo ya utafutaji wa masoko ifikapo Juni 2035.	2035	**10,000**	**WVB** MoF, TAMISEMI, SIDO, COSTECH, TIRDO, NEEC, TPSF, CAMARTEC, TEMDO, Taasisi za utafiti na Elimu, Washirika wa Maendeleo na Taasisi zingine za Umma.
		Kuimarisha uhusiano baina ya wajasiriamali wadogo na wa kati na kampuni kubwa.	Kuunganisha jasiriamali ndogo na za kati 1,900,000 na kampuni za ndani ifikapo Juni 2035.	2035	**5,500**	**WVB** MoF, TAMISEMI, SIDO, COSTECH, TIRDO, NEEC, TPSF, CAMARTEC, TEMDO, Taasisi za utafiti na Elimu, Washirika wa Maendeleo na Taasisi zingine za Umma.
			Kuunganisha jasiriamali ndogo na za kati 500,000 na kampuni za nje ifikapo Juni 2035	2035	**7,500**	**WVB** MoF, TAMISEMI, SIDO, COSTECH, TIRDO, NEEC, TPSF, CAMARTEC, TEMDO, Taasisi za utafiti na Elimu, Washirika wa Maendeleo na Taasisi zingine za Umma.
		Kuimarisha taasisi za utafutaji masoko zinazosaidia jasiriamali ndogo na za kati.	Kuzijengea uwezo taasisi tatu (3) za masoko zinazowezesha jasiriamali ndogo na za kati ifikapo Juni 2035.	2035	**9,000**	**WVB** MoF, TAMISEMI, SIDO, COSTECH, TIRDO, NEEC, TPSF, CAMARTEC, TEMDO, Taasisi za utafiti na Elimu, Washirika wa Maendeleo na Taasisi zingine za Umma.

Na	Malengo	Mikakati	Shabaha	Muda	Rasilimali Fedha (Shs. Mil)	Watekelezaji
6	Kujumuisha masuala mtambuka katika shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati.	Kujenga uelewa wa masuala ya mazingira na fursa zilizopo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati.	Jasiriamali 6,000,000 kupata uelewa wa hatua za kulinda mazingira ifikapo Juni 2035.			
		Kuwezesha upatikanaji na matumizi ya teknolojia rafiki za mazingira kwa wajasiriamali wadogo na wa kati.	Jasiriamali 1,500,000 kutumia teknolojia rafiki za mazingira ifikapo Juni 2035.	2035	**1,000**	**WVB** OMR - Mazingira, SIDO, NEMC
		Kuhamasisha ushiriki wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika shughuli za ujasiriamali.	Wanawake wajasiriamali 1,000,000 kupata mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara ifikapo Juni 2035;	2035	**1,000**	**WVB** OWM-KVAM, MSGWS
			Vijana wajasiriamali 3,500,000 kupata mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara ifikapo Juni 2035.	2035	**1,500**	**WVB** OWM-KVAM, MSGWS
			Wajasiriamali wenye ulemavu 500,000 kupata mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara ifikapo Juni, 2035.	2035	**1,000**	**WVB** OWM-KVAM, MSGWS
			Wanawake wajasiriamali 1,000,000 kupata huduma za kifedha ifikapo Juni 2035.	2035	**1,500**	**WVB** OWM-KVAM, MSGWS

Na	Malengo	Mikakati	Shabaha	Muda	Rasilimali Fedha (Shs. Mil)	Watekelezaji
			Vijana wajasiriamali 3,500,000 kupata huduma za kifedha ifikapo Juni 2035;	2035	**1,000**	**WVB** OWM-KVAM, MSGWS
			Wajasiriamali wenye ulemavu 500,000 kupata huduma za kifedha ifikapo Juni 2035.	2035	**1,500**	**WVB** OWM-KVAM, MSGWS
		Kuhamasisha ujumuishaji wa masuala ya VVU/UKIMWI na magonjwa yasiyoambukizwa katika shughuli za ujasiriamali.	Wajasiriamali 3,000,000 kupata uelewa kuhusu VVU/UKIMWI ifikapo Juni 2035.	2035	**2,000**	**WVB** MoH
			Wajasiriamali 1,000,000 kupata uelewa kuhusu magonjwa yasiyoambukizwa ifikapo Juni 2035	2035	**2,000**	**WVB** MoH
		JUMLA			**1,786,500**	

SURA YA SITA

6. MFUMO WA KITAASISI, UFUATILIAJI NA TATHMINI

6.1. Mfumo wa Kitaasisi

Mfumo wa kitaasisi hubainisha majukumu makuu ya taasisi na wadau wengine wakuu wanaoandaa nyenzo za utekelezaji, usimamizi, ufuatiliaji, na tathmini ya utekelezaji wa sera ili kuhakikisha matokeo yaliyokusudiwa yanafikiwa. Wadau wakuu ni wizara, idara na wakala za serikali; mamlaka za serikali za mitaa; sekta binafsi; washirika wa maendeleo; taasisi za utafiti; Asasi Zisizo za Serikali (AZISE); vyombo vya habari na jamii kwa ujumla. Majukumu ya wadau hao yanafanuliwa hapa chini.

6.2. Majukumu ya Wadau katika Utekelezaji wa Sera

(i) Wizara yenye dhamana ya uendelezaji Jasiriamali Ndogo na za Kati

Wizara yenye dhamana ya uendelezaji jasirimali ndogo na za kati itakuwa mratibu mkuu wa utekelezaji, ufuatiliaji, tathmini na mapitio ya sera kwa vipindi maalumu ili kuhakikisha malengo ya sera yanafikiwa. Aidha, Wizara itaandaa na kuchapisha taarifa ya utekelezaji wa sera.

(ii) Wizara yenye dhamana ya Fedha

Wizara yenye dhamana ya fedha kwa kushirikiana na wadau wengine, itawezesha upatikanaji wa rasilimali fedha ili kufanikisha utekelezaji wa Sera.

(iii) Wizara yenye dhamana ya Uwekezaji

Wizara yenye dhamana ya uwekezaji itaweka mazingira wezeshi kwa ajili ya maendeleo jasiriamali ndogo na kati.

(iv) Wizara yenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

TAMISEMI itakuwa na jukumu la kuratibu utekelezaji wa sera katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

(v) Wizara za sekta nyingine

Wizara za sekta nyingine zitasaidia utekelezaji wa Sera kwa kujumuisha masuala ya uendelezaji jasiriamali ndogo na kati katika mikakati, mipango na miradi yao.

(vi) Idara na Wakala za Serikali

Idara na Wakala za Serikali zitakuwa na jukumu la kuhakikisha masuala ya uendelezaji jasiriamali ndogo na kati yanajumuishwa katika mikakati ya maendeleo, mipango, na programu zao.

(vii) Sekretarieti za Mikoa

Sekretarieti za Mikoa zitakuwa na jukumu la kuratibu masuala yote ya shughuli za uendelezaji jasiriamali ndogo na kati katika mikoa husika.

(viii) Mamlaka za Serikali za Mitaa

Mamlaka za Serikali za Mitaa zitakuwa na majukumu ya kutekeleza masuala yote ya uendelezaji jasiriamali ndogo na kati katika maeneo yao; kuhakikisha masuala ya uendelezaji jasiriamali yanajumuishwa katika mikakati yao ya maendeleo; na kuhamasisha jamii kutumia fursa zilizopo katika maeneo yao.

(ix) Mashirika ya Sekta Binafsi

Mashirika ya sekta binafsi yatakuwa na jukumu la kuwezesha maendeleo ya jasiriamali ndogo na kati na kuishauri Serikali katika masuala hayo.

(x) Washirika wa Maendeleo

Washirika wa Maendeleo watakuwa na jukumu la kusaidia jitihada za Serikali katika kujenga sekta imara na shindani ya uendelezaji jasiriamali ndogo na kati; kuhamasisha maendeleo endelevu ya sekta hiyo; na kutekeleza hatua za kimkakati za shughuli za uendelezaji jasiriamali. Vilevile, watashirikiana na Serikali katika nyanja mbalimbali zinazohitaji msaada wa kitaalamu na kifedha.

(xi) Taasisi za Utafiti

Taasisi za utafiti zitakuwa na jukumu la kutoa ujuzi na maarifa yanayokidhi mahitaji ya wajasiriamali wadogo na wa kati ikiwa ni pamoja na kubuni teknolojia rahisi zitakazotumiwa na wajasiriamali wadogo na wa kati na kufanya utafiti wa soko kwa lengo la kuwajulisha fursa zilizopo.

(xii) Taasisi za Elimu

Taasisi za Elimu zitakuwa na jukumu la kuandaa programu za mafunzo ya kuwajengea uwezo wajasiriamali wadogo na wa kati.

(xiii) Asasi Zisizo za Serikali

Asasi zisizo za Serikali zitakuwa na jukumu la kutafuta rasilimali, kutoa elimu, ujuzi na maarifa kuhusu uendelezaji wa jasiriamali ndogo na kati.

(xiv) Vyombo vya Habari

Vyombo vya habari vitakuwa na jukumu la kuelimisha na kuhamasisha wadau na umma kwa ujumla kuhusu umuhimu wa kushiriki katika shughuli za uendelezaji wa jasiriamali ndogo na kati na kueleza fursa zilizopo katika sekta hiyo.

(xv) Jamii

Jamii itachangamkia fursa zilizopo katika uendelezaji wa jasiriamali ndogo na kati kwa kushiriki katika mafunzo ya biashara; kutumia bidhaa zinazotokana na jasiriamali ndogo na za kati; na kuhamasisha maendeleo ya jasiriamali ndogo na za kati katika maeneo yao.

SURA YA SABA

7. MFUMO WA UFUATILIAJI NA TATHMINI

7.1. Utangulizi

Sehemu hii inafafanua umuhimu wa kufanya ufuatiliaji na tathmini ya Sera na mfumo wa ufuatiliaji na tathmini. Ufuatiliaji na tathmini ni nyenzo muhimu inayosaidia kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera. Nyenzo hii huwezesha Wizara yenye dhamana kupima ufanisi wa utekelezaji wa malengo yaliyobainishwa kwenye Sera. Aidha, mfumo huu husaidia Wizara yenye dhamana kuratibu utekelezaji wa mikakati kwa kubuni programu mbalimbali. Sura hii inaelezea namna dira ya Sera itakavyofikiwa kupitia utekelezaji wa mkakati na jinsi wadau watakavyonufaika na utekelezaji huo. Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini unaonesha lengo kuu la mkakati; walengwa wa afua mbalimbali zitazotekelezwa; mpango wa ufuatiliaji; mapitio yaliyokusudiwa; mpango wa tathmini; na mpango wa utoaji taarifa.

7.2. Lengo kuu

Lengo kuu la Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ni kutoa mwongozo wa utekelezaji wa mkakati ili kuongeza ufanisi na tija katika afua zinazotekelezwa. Malengo mahususi ya mfumo huu ni kama ifuatavyo:

(i) Kuweka viashiria vya kuwezesha tathmini ya utekelezaji;
(ii) Kuweka mwongozo wa ushiriki wa wadau katika shughuli za utekelezaji na ufuatiliaji; na
(iii) Kudhibiti matumizi ya rasilimali wakati wa utekelezaji.

7.3. Walengwa

Walengwa wa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ni Wizara za Kisekta, sekretarieti za mikoa, mamlaka za serikali za mitaa, sekta binafsi, Asasi za Kiraia (AZAKI), taasisi za elimu na utafiti na jamii kwa ujumla.

7.4. Mipango ya Ufuatiliaji, Mapitio na Tathmini

Sehemu hii inafafanua mpango wa ufuatiliaji, mapitio na tathmini kwa kipindi cha miaka 10 cha utekelezaji wa mkakati. Vilevile, sehemu hii inaeleza kuhusu mapitio ya sera yatakayofanyika ya mara kwa mara; upimaji na tathmini ya ufanisi; tija; manufaa na uendelevu wa matokeo ya mpango.

7.4.1. Mpango wa Ufuatiliaji

Ufuatiliaji utahusisha ukusanyaji endelevu wa data, uchambuzi, viashiria vya upimaji na muda wa uwasilishaji taarifa. Mpango huu utaiwezesha Wizara yenye dhamana pamoja na wadau kupata taarifa ya mwenendo wa utekelezaji kwa lengo la kufanya tathmini ya utekelezaji na kiwango cha matumizi ya fedha zilizotengwa katika kipindi maalumu.

7.4.2. Mpango wa Mapitio

Mpango wa mapitio utatekelezwa na Wizara yenye dhamana kwa kushiriana na wadau mbalimbali ambao utajumuisha mikutano ya mapitio itakayofanyika, mapitio ya utekelezaji wa viashiria vya muda mfupi na tathmini za papo kwa papo. Mpango utasaidia mamlaka zinazohusika kufanya uamuzi sahihi, na kuongeza uwazi na uwajibikaji kwa wadau.

7.4.2.1. Mpango wa Mapitio ya Viashiria vya Muda Mfupi

Mpango huu unatumia vigezo vinavyotumika kubaini matukio muhimu katika ratiba, kama vile kukamilika kwa matukio makuu au hatua zilizoainishwa wakati wa upangaji. Hivyo, mapitio ya viashiria vya muda mfupi yanalenga kutathmini kiwango cha utekelezaji wa malengo kwa mwaka unaohusika na kubaini ikiwa utekelezaji uko katika mwelekeo sahihi au la. Taarifa ya mapitio haya itawezesha kufanyika maboresho ya malengo na mikakati ya kuyafikia.

7.4.3. Mpango wa Tathmini

Tathmini ya utekelezaji itafanyika kwa vipindi maalumu ili kubaini ufanisi na tija ya utekelezaji wa malengo. Mchakato wa tathmini utajikita katika kupima matokeo yaliyopatikana na manufaa yake kwa walengwa. Katika kipindi cha utekelezaji wa Sera, tathmini itafanyika kwa vipindi viwili, ambapo tathmini ya kwanza itafanyika baada ya miaka 5 na tathmini ya pili itafanyika baada ya miaka 10. Tathmini zitapima kufikiwa kwa malengo na shabaha zilizoainishwa katika Sera ya Maendeleo ya Jasiriamali Ndogo na za Kati ya mwaka 2003 (Toleo la mwaka 2025). Vilevile, tathmini hizo zitabainisha changamoto za utekelezaji na kuzifanyia kazi. Viashiria vya ufuatiliaji na tathmini vinabainishwa katika jedwali Na. 2.

***Jedwali Na. 2:* Viashiria vya Utuatiliaji na Tathmini**

Viashiria vya Matokeo ya Muda Mfupi	Viashiria vya Matokeo ya Muda Mrefu	Takwimu Msingi	Chanzo
Lengo 1: Kuimarisha miundombinu wezeshi ya shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati			
Idadi ya Majengo ya Viwanda	Badiliko la idadi ya wajasiriamali wadogo na wa kati	Milioni 6	i. Taarifa za OWM-TAMISEMI ii. Taarifa za Wizara ya Viwanda na Biashara
Badiliko la asilimia ya maghala ya kuhifadhia bidhaa			
Badiliko la asilimia ya biashara rasmi	(ii) Badiliko la idadi ya jasiriamali ndogo na za kati zilizosajiliwa.	16,489	
Idadi ya mita za mraba kwa maeneo yaliyotengwa			
Idadi ya vituo atamizi			
Idadi ya kongani za viwanda			
Kuwapo kwa mwongozo wa urasimishaji biashara			
Kuwapo kwa Mwongozo wa Mafunzo ya Ujasiriamali uliohuishwa			
Lengo 2: Kuimarisha ukuaji wa jasiriamali ndogo na za kati mijini na vijijini			
Idadi ya wajasiriamali waliopata mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara	(i) Badiliko la kiwango cha jasiriamali ndogo na za kati zinazofungwa kwa mwaka; na	Takwimu zitaainishwa baada ya kufanya utafiti wa msingi.	i. Taarifa za OWM-TAMISEMI ii. Taarifa za Wizara ya Viwanda na Biashara iii. Taarifa za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
Badiliko la asilimia ya biashara rasmi			
Idadi ya vituo atamizi			
Kuwapo kwa mwongozo wa urasimishaji biashara			
Kuwapo kwa Mwongozo wa Mafunzo ya Ujasiriamali uliohuishwa			
Lengo 3: Kuongeza matumizi ya teknolojia na ubunifu kwa wajasiriamali wadogo na wa kati			
Idadi ya vituo vya kuendeleza teknolojia	(i) Badiliko la ubora na aina za bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali wadogo na wa kati;	Takwimu zitaainishwa baada ya kufanya utafiti wa msingi.	i. Taarifa za Wizara ya Viwanda na Biashara ii. Taarifa za Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari
Idadi ya mitambo iliyozalishwa kwa mwaka			
Idadi ya vipuri vilivyozalishwa kwa mwaka			
Idadi ya ubunifu wa teknolojia kwa mwaka			

Viashiria vya Matokeo ya Muda Mfupi	Viashiria vya Matokeo ya Muda Mrefu	Takwimu Msingi	Chanzo
Badiliko la asilimia ya matumizi ya TEHAMA	(ii) Badiliko la idadi ya jasiriamali ndogo na za kati zinazotumia biashara-mtandao	5,040,000	
Lengo 4: Kuwezesha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wajasiriamali wadogo na wa kati.			
Badiliko la idadi ya mikopo iliyotolewa	(i) Kiwango cha upatikanaji wa huduma za mitaji kwa wajasiriamali wadogo na wa kati.	Tsh 3.63 trilioni	i. Taarifa za Wizara ya Fedha ii. Taarifa za Wizara ya Viwanda na Biashara
Badiliko la idadi ya jasiriamali ndogo na za kati zilizounganishwa na taasisi za kifedha			
Badiliko la idadi ya biashara changa zilizopata mitaji kutoka kwenye taasisi za fedha			
Lengo 5: Kuwezesha upatikanaji wa masoko ya bidhaa na huduma zinazozalishwa na wajasiriamali wadogo na wa kati			
Idadi ya wajasiriamali walioshiriki maonesho ya ndani kwa mwaka	(i) Badiliko la kiwango cha mauzo katika soko kwa bidhaa zilizozalishwa na jasiriamali ndogo na za kati katika soko la kitaifa, kikanda na kimataifa	Tsh. 1,224,981,950	i. Taarifa za Wizara ya Viwanda na Biashara
Idadi ya taasisi zilizojengewa uwezo			
Badiliko la asilimia ya biashara ndogo zilizounganishwa na kampuni za ndani			
Badiliko la asilimia ya biashara ndogo zilizounganishwa na kampuni za nje			
Badiliko la asilimia ya wajasiriamali waliopata mafunzo ya utafutaji masoko			
Lengo 6: Kujumuisha masuala mtambuka katika shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati.			
Badiliko la asilimia ya wajasiriamali wadogo waliopewa elimu ya utunzaji wa mazingira	(ii) Kiwango cha wajasiriamali kuzingatia utunzaji wa mazingira	Takwimu zitaainishwa baada ya kufanya utafiti wa msingi.	i. Taarifa za Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira ii. Taarifa za Wizara ya Viwanda na Biashara

Viashiria vya Matokeo ya Muda Mfupi	Viashiria vya Matokeo ya Muda Mrefu	Takwimu Msingi	Chanzo
Badiliko la asilimia ya wanawake wajasiriamali waliopata mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara	(iii) Badiliko la idadi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wanaojihusisha na shughuli za ujasiriamali	78,984	i. Tarifa za Ofisi ya Waziri Mkuu-Kazi, Vijana, Ajira na Mahusiano ii. Taarifa za Wizara ya Viwanda na Biashara iii. Taarifa za Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu
Badiliko la asilimia ya vijana wajasiriamali waliopata mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara			
Badiliko la asilimia ya wajasiriamali wenye ulemavu waliopata mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara			
Badiliko la asilimia ya wanawake wajasiriamali waliopata huduma za kifedha			
Badiliko la asilimia ya vijana wajasiriamali waliopata huduma za kifedha			
Badiliko la asilimia ya wajasiriamali wenye ulemavu waliopata huduma za kifedha			
Badiliko la asilimia ya wajasiriamali waliopata uelewa kuhusu VVU/UKIMWI	(iv) Badiliko la kiwango cha watu wenye VVU/UKIMWI na magonjwa yasiyoambukizwa kwa wajasiriamali	Takwimu zitaainishwa baada ya utafiti wa msingi kufanyika.	i. Taarifa za Wizara ya Afya ii. Taarifa za Wizara ya Viwanda na Biashara
Badiliko la asilimia ya wajasiriamali waliopata uelewa kuhusu magonjwa yasiyoambukizwa			

7.4.4. Mpango wa utoaji taarifa

Mpango huu utahusisha utoaji taarifa kuhusu mwenendo wa ufikiwaji wa malengo yaliyobainishwa katika Sera ya Maendeleo ya Jasiriamali Ndogo na za Kati ya mwaka 2003 (Toleo la mwaka 2025) ukilinganisha matumizi ya rasilimali na manufaa yaliyopatikana kwa walengwa. Vilevile, mpango huu utahusisha utoaji wa taarifa ndani na nje ya Wizara yenye dhamana ya jasiriamali ndogo na za kati.

7.4.4.1. Mpango wa utoaji taarifa ndani ya Wizara

Mpango wa utoaji taarifa ndani ya Wizara unakusudiwa kutoa muhtasari wa maendeleo ya utekelezaji wa Sera. Kipekee, mpango huu utahusisha maandalizi ya aina nne za taarifa, yaani taarifa za maendeleo ya idara; taarifa za maendeleo ya miradi; taarifa za kila robo mwaka; na taarifa za kila mwaka. Taarifa hizi zitaandaliwa katika vipindi vya robo mwaka; mwaka au wakati mwingine kwa kadri itakavyohitajika.

7.4.4.2. Mpango wa utoaji taarifa nje ya Wizara

Mpango wa utoaji wa taarifa nje ya Wizara utahusisha maandalizi ya taarifa za fedha, taarifa za kila mwaka, taarifa za vipindi vya kati na taarifa za matokeo ya utekelezaji. Utoaji wa taarifa hizi utabainisha aina ya taarifa; wapokeaji; muda wa utoaji taarifa; na taasisi zitakazowajibika kutoa aina tofauti ya taarifa. Taarifa hizi zitawasilishwa kwa wadau kama vile Wizara, Bunge na umma kwa ujumla.

7.5. Ukusanyaji na Uchambuzi wa Data

Data za ufuatiliaji na tathmini zitakusanywa mara kwa mara kwa kutumia zana za ufuatiliaji zilizokubaliwa na Wizara yenye dhamana. Data zitakusanywa kupitia tafiti, taarifa za utendaji, taarifa kuhusu shughuli mahususi za utekelezaji wa Sera, ziara za ufuatiliaji na vyanzo vingine vinavyoaminika. Data zitachambuliwa na kuingizwa kwenye kanzidata ya Taifa ya jasiriamali ndogo na za kati.

7.6. Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini

7.6.1. Aina za taarifa za ufuatiliaji na tathmini

Katika ngazi ya Wizara, taarifa mbalimbali zitatumika kufanya ufuatiliaji na tathmini kama ifuatavyo:

(i) Taarifa za Wizara yenye dhamana za kila robo mwaka, nusu mwaka na kila mwaka;
(ii) Taarifa za tathmini za wizara, idara na wakala za serikali, mashirika, mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
(iii) Taarifa za kila mwaka za washirika wa maendeleo; na
(iv) Taarifa za mapitio ya Sera na tafiti mbalimbali.

7.6.2. Ratiba ya utoaji taarifa

Aina ya Taarifa	Maudhui	Muda
Taarifa ya kina ya utekelezaji	Taarifa za kina zinazojumuisha shughuli zote zilizotekelezwa katika ngazi ya Wizara	Nusu mwaka na mwaka
Taarifa ya tathmini	Taarifa za tathmini ya utekelezaji za ndani na nje ya Wizara	Miaka mitano; na miaka kumi
Mapitio ya utekelezaji wa Sera	Mapitio ya utekelezaji wa Sera	Baada ya miaka mitano

7.6.3. Mfumo wa utoaji taarifa

Taarifa za utekelezaji zitaandaliwa na taasisi zinazohusika na kuwasilishwa kwa Wizara yenye dhamana kwa ajili ya kuziunganisha. Aidha, Wizara itaandaa taarifa za utendaji na kuziwasilisha kwa wadau kila robo mwaka, nusu mwaka na kila mwaka kwa hatua muhimu za utekelezaji.

7.6.4. Mfumo wa kutoa mrejesho

Mfumo wa utoaji mrejesho unahusisha utaratibu wa kubadilishana taarifa baina ya watekelezaji na watumiaji wa taarifa. Aidha, mrejesho utaimarisha ushirikiano baina ya wadau ili kuboresha taarifa na mifumo ya utoaji taarifa.

7.7. Matumizi ya Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini

Taarifa za ufuatiliaji na tathmini zitatumiwa na wadau ili:


(i) Kuwezesha utoaji bora wa huduma;
(ii) Kuboresha uwajibikaji kupitia matokeo yatakayopatikana;
(iii) Kusaidia Wizara kufanya uamuzi sahihi;
(iv) Kuandaa mipango; na
(v) Kuhakikisha kunakuwa na matumizi sahihi ya rasilimali.

7.8. Mpango wa Utekelezaji

Mpango wa kina wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jasiriamali Ndogo na za Kati ya mwaka 2003 (Toleo la mwaka 2025) unaojumuisha maeneo sita ya kipaumbele yaliyobainishwa katika sera na mkakati wake wa utekelezaji utaandaliwa baada ya Sera kupitishwa. Mikakati mbalimbali iliyoobainishwa itaandaliwa ili kubainisha shughuli na gharama za utekelezaji. Aidha, watekelezaji wa mpango watatumia njia shirikishi na jumuishi na hivyo kufikia lengo kuu la Sera ambalo ni kuongeza mchango wa shughuli za ujasiriamali katika maendeleo ya uchumi nchini.

7.9. Hitimisho

Ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa ni zana muhimu zitakazotumiwa na Wizara yenye dhamana na wadau wengine kufanya uamuzi na kuimarisha uwajibikaji na uwazi wakati wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jasiriamali Ndogo na za Kati ya Mwaka 2003 (Toleo la mwaka 2025).



Wizara ya Viwanda na Biashara,
Mji wa Serikali – Mtumba,
Mtaa wa Viwanda, S.L.P 2996,
40478 Dodoma,
Tovuti: www.viwanda.go.tz